



## **Wito wa Amani na Utulivu kutoka kwa Akina mama nchini Kenya**

**Mwanzo.** Wiki mbili zilizopita zimekuwa za kuvunja moyo sana kwa Wakenya na kuhuzunisha zaidi kwa akina mama nchini Kenya. Ulimwengu ultazama kwa mshangao, na kwa masikitiko Kenya ikimwaga damu kutokana na vitendo vya fujo na uvunjaji wa sheria vilivofanywa na baadhi ya raia. Hii imeiweka nchi yetu katika hali ya sintofahamu - na kutishia kulemaza uchumi wetu ambaao tayari umedhoofika. Matendo kama hayo hayatuletei mema kama taifa, badala yake yanatuletea tisho kubwa kwa watoto wetu na vizazi vijavyo.

Kama akina mama nchini Kenya, tuna wasiiasi mkubwa na tunaungana pamoja na akina mama wenzetu wanaoomboleza vifo vya wapendwa wao, majeruhi na kupoteza mali kwa njia zisizofaa. Tunazihurumia familia na kuwaombea faraja kutoka kwa Mungu. Ni kwa sababu hii ambapo tunatoa taarifa hii.

Tunaanza taarifa hii kwa kuwakumbusha Wakenya wote kwamba Mungu ametujalia nchi nzuri sana, nchi ambayo inaenziwa na kuheshimiwa na watu wengi duniani kote. Kenya ina rasilimali za kibinadamu, wanyamapori, miundombinu ya ajabu ya barabara na uvumbuzi wa kiteknolojia ya kiwango cha kimataifa kama vile MPESA, mionganoni mwa zingine. Kwa ufupi, tumepiga hatua sana katika mambo mengi. Mwenendo usiofaa tulioshuhudia kutoka kwa baadhi ya watu wetu hivi karibuni na ambaao umesababisha vifo na uharibifu wa mali haukulaliki kamwe.

Vivyo hivyo, matumizi ya nguvu kupita kiasi na baadhi ya walinda usalama katika kujaribu kudumisha amani na kuzima fujo hayakubaliki pia. Kwa sababu ya matukio hayo, Wakenya wengi wana huzunika huku wengine wakiwa na uwoga.

Ni kweli kwamba gharama ya maisha imepanda. Wakenya wengi hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, huduma za matibabu, mafuta na mahitaji mengine. Kutokana na hayo, Wakenya wana njaa na ghadhabu. Tunatoa wito wa amani na utulivu. Tunajua kuwa, sisi ni watu wanaoamini Mungu. Hivi karibuni mambo yatabadilika na yaye mazuri.

Kama akina mama nchini Kenya, tungependa kuwafahamisha Wakenya wote kwamba kama demokrasia ya kikatiba, Kenya ni nchi inayoongozwa na utawala wa kisheria. Kwa hivyo, kila mtu anatarajiwa kufuata sheria. Ni muhimu kuwa



Wakenya watoe nafasi kwa mazungumzo ili tujenge uchumi wetu na taifa kwa pamoja.

Akina mama nchini Kenya tunafahamu na kutambua kwamba Katiba ya Kenya inampa kila raia wa Kenya haki ya kukusanyika, kuandamana na kuwasilisha malalamishi yake. Hata hivyo, tunajikumbusha na kujitahadharisha kuwa utekelezaji wa haki hizi unapaswa kufanya ndani ya mipaka ya kikatiba.

Mwisho, tunaunga mkono kikamilifu Katiba yetu ambayo inaweka wazi wajibu wa juu zaidi wa kulinda haki za kibinadamu na uhuru wa kimsingi na utawala wa kisheria kwa Rais aliye mamlakani. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa Rais, Mheshimiwa William Samoei Ruto kulinda maisha ya Wakenya wote na mali zao kwa mujibu wa Katiba ambayo aliapa kuitetea.

Kama akina mama nchini Kenya, tunajitolea kuendelea kuombea amani na ustawi wa taifa letu na watu wetu. Tunahisi maumivu ya wale wote ambao wameathiriwa na janga hili, na kwa hakika, tunaomba kuwa maneno ya Wimbo wetu wa Taifa yawafae: '*Kenya Istahili Heshima*'

Dkt. Jennifer N. Riria

PhD, EBS, MBS, HRH/Balozi wa Nia Njema, ICON/HP

Mwenyekiti wa Bewa la AWLN Kenya & Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ENA

*Imetiwa saini tarehe 17 Julai 2023 na Dkt. Jennifer Riria kwa niaba ya Akina mama nchini Kenya chini ya mwavuli wa ENA, AWLN, WMN-K, DTF*